# TAARIFA KWA UMMA

## UWEPO WA VYETI VYA KIELEKTRONIKI VYA WATOA DAWA WA MADUKA YA DAWA MUHIMU (ADDO DISPENSERS)

**DODOMA: MEI 18, 2023**

Mafunzo ya watoa dawa wa Maduka ya Dawa Muhimu (DLDM) yalianza kutolewa Mwaka 2003. Hadi kufikia Mwaka 2022, watoa dawa **23,848** walikuwa wamepatiwa mafunzo na vyeti vya utoaji dawa. Aidha, Mwezi Aprili 2022, Wizara ilisitisha mafunzo hayo ili kufanya tathmini ya hali ya utoaji dawa nchini kupitia maduka ya dawa.

Katika kuboresha mifumo ya huduma na usimamizi wa utoaji dawa kwenye maduka ya dawa, Baraza la Famasi limeboresha vyeti vya watoa dawa sambamba na kufanya uhakiki wa vyeti katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Uhakiki huu ni kutokana na wimbi la vyeti vya kugushi ambavyo vimekuwa vikitolewa na kutumika na watu wasio waaminifu.

Zoezi la maboresho lilianza Mwaka 2019 na limekamilika ambapo kwa sasa vyeti vyote vya watoa dawa vinatolewa kwa mfumo wa kielektroniki. Katika uhakiki huu, jumla ya watoa dawa 27,980 walijitokeza kuhakikiwa kati ya hao, 23,848 ( 85%) walikidhi vigezo na kupatiwa vyeti vya kielektoniki, **1850 (7%)** walibainika kughushi vyeti, **2282 (8%)** waliwasilisha nyaraka zenye upungufu na kuna ambao hawakujitokeza hadi zoezi lilipokamilika. Hadi kufikia Desemba, 2022 vyeti vya watoa dawa wa **DLDM 23,848** vimeandaliwa na kupelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuwakabidhi wahusika.

Kwa maelezo hayo, kwa wale wote ambao watahitaji kuhakikiwa wafike Ofisi za Baraza la Famasi Makao Makuu AU Ofisi za Kanda ili kufanyiwa uhakiki kabla ya zoezi hilo kuhitimishwa tarehe 30 Juni, 2023 ambapo vyeti vya zamani havitatambuliwa na vitakuwa vimefutwa rasmi.

**WITO:** Tunatoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanapata huduma za dawa katika maduka yaliyosajiliwa na yenye watoa dawa waliothibitishwa na kutambuliwa na Baraza. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe ***info@pc.go.tz*** au kwa simu bila malipo **0800 110015.**

**Elizabeth Shekalaghe**
**Msajili - Baraza la Famasi**